MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

**Na: 2. Msimu wa Kilimo 2019/20** **Tathmini Oktoba 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Oktoba 21-31, 2019**

**Muhtasari**


- Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, wakulima wanaendelea na shughuli kuandaa mashamba na kupanda isipokuwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa kagera ambapo mazao yaliyopandwa mwanzoni mwa msimu wa vuli yako katika hatua ya palizi.
- Kutokana na hali ya ukavu wa muda mrefu kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua na nyanda za juu kaskazini mashariki wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2019

Katika siku kumi zilizopita za mwezi Octoba, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika kipindi hiki ikilinganishwa na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ambayo iliendelea kuimarika. Hali ya kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa ilipelekea kuendelea kuusogeza ukanda wima wa mvua maeneo yanayozunguka ukanda wa Ziwa Victoria. Hali hii ilisababisha uwepo wa mvua na upepo hafifu hadi wa wastani katika maeneo mengi ya nchi. Uwepo wa joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hasa katika pwani ya Afrika mashariki liliendelea kusababisha mvua katika maeneo mengi ya nchi hasa pwani ya kaskazini. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliripotiwa katika maeneo ya pwani ya Angola hivyo ilisababisha uwepo wa mchango mdogo kwenye mifumo ya utengenezaji wa mvua katika upande wa magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2019

Katika dikadi hii vipindi vya mvua za wastani viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini. Aidha mvua nyepesi iliripotiwa katika maeneo ya pwani ya kusini, nyanda za juu kusini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi. Kiasi cha mvua kilichoripotiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi ni kuanzia milimita 26 na zaidi ya milimita 250 kama inavyoonesha katika ramani.




**Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Oktoba 11- 20, 2019.**

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2019

Katika kipindi cha dekadi iliyopita wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli waliendelea na uandaaji wa mashamba pamoja na upandaji, Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa msimu wa kilimo unaozotarajiwa kuanza mwezi Novemba hadi Disemba. Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa si ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi, hii ni kutokana na kuwepo kwa vipindi vya ukavu.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuimalika husussan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hata hivyo katika kipindi cha mwanzo kunatarajiwa kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa iliyopo kusini mwa dunia hivyo kupelekea kuchelewesha kwa ukanda wa mvua kuelekea kusini. Pia upepo kutoka mashariki na kaskazini mashariki unatarajiwa kuvuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha uwepo wa hewa yenye unyevunyevu, pia uwezekano wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa baharini kwa kipindi hiki unatarajiwa hasa eneo la kusini mashariki mwa Madagascar. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kuwa na mchango mdogo kwenye mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua za wastani katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) kunatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kupata hali ya ukavu.

## HALI YA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Mvua zinatarajiwa kuongezeka katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan kanda ya ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi. Wakulima wa maeneo husika wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kupanda pale kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Hata hivyo wakulima katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki wanashauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame kutokana na mvua za wastani hadi chini ya wastani zinazotarajiwa. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, wakulima wanashauriwa kutozitumia mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha kwa uoteshaji wa mazao bali waendelee na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya mvua msimu zinazotarajiwa kuanza kati ya mwezi Novemba na Desemba. Hali ya ukavu inayotarajiwa itaathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa maeneo mengi nchini hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hivyo wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito inatarajiwa kuongezeko kidogo katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la ziwa Viktoria. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro,** Dar es Salaam-Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***